

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YA HUDUMA ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA IGUNGA (“IGUNGA WSSA”) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-046

Mnamo tarehe 5 Mei 2019, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Igunga (Igunga WSSA) ya kuomba kurekebisha bei za huduma za majisafi kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Jedwali namba 1 hadi 3 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (Shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizopendekezwa					
		2018/19	Badilik o	2019/20	Badilik o	2020/21	Badilik o
Majumbani	855	32%	1,131	16%	1,311	5%	1,381
Taasisi	1,125	30%	1,457	9%	1,587	6%	1,687
Biashara	1,415	24%	1,750	9%	1,910	7%	2,040
Viwanda	1,415	24%	1,750	9%	1,910	7%	2,040
Magati	1,500	25%	1,870	7%	2,000	10%	2,200
Wateja Wakubwa	3,280	5%	3,460	13%	3,920	8%	4,230

Jedwali 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa		
		2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani				
Taasisi				
Biashara				
Viwandani				
Magati				
	Asilimia 20 ya Jumla ya Gharama za Maunganisho Mapya ya Maji.		Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvukazi kama ilivyobainishwa katika Kanuni za Maji za Mwaka 2013	

Wateja Wakubwa		
-------------------	--	--

Jedwali 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Tozo Zinazopendekezwa					
		2018/19	Badilik o	2019/20	Badiliko	2020/21	Badilik o
Majumbani	10,000	0%	10,000	50%	15,000	0%	15,000
Taasisi	10,000	0%	10,000	100%	20,000	0%	20,000
Biashara	10,000	0%	10,000	100%	20,000	0%	20,000
Viwandani	10,000	0%	10,000	150%	25,000	0%	25,000
Magati	0	-	0	-	0	-	0
Wateja Wakubwa	0	-	0	-	0	-	0

Kwa mujibu wa wasilisho la Igunga WSSA, bei, ada na tozo zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kupata mapato ya kutosha kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo. Igunga WSSA imebainisha kuwa mabadiliko ya bei na tozo yanayopendekezwa yataiwezesha Mamlaka kumudu gharama za uendeshaji zilizoongezeka, kuboresha huduma za maji safi ikiwa ni pamoja na kuongeza mtandao wa majisafi na kufanya uwekezaji wa miundombinu ya maji na hivyo kuboresha utoaji wa huduma ya maji safi katika mji wa Igunga.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 13 Juni 2019, katika Ukumbi wa Sakao Modern Mjini Igunga** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu kabla ya tarehe **20 Juni 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Ofisi za UWURA **GHOROFA YA NNE, JENGO LA PSSSF, MTAA WA MAKOLE, S.L.P 2857 DODOMA** au Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira **IGUNGA** zilizopo mjini **Igunga**.

Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
15 Mei 2019